THE NATIONAL TREASURY
& PLANNING

REPUBLIC OF KENYA

MWONGOZO WA

MWANANCHI

Bajeti ya Mwaka Wa 2022/23

Chapisho la Hazina ya Kitaifa na Mipango

Hazina ya Kitaifa na Mipango
@KeTreasury
communications@treasury.go.ke
www.treasury.go.ke

YALIYOMO

Ukurasa wa 2
Mada: Kuharakisha Ufufuaji Uchumi kwa Maisha Bora ya Wakenya

Ukurasa wa 3
Matumizi Muhimu

Ukurasa wa 4
Hali ya Uchumi

Ukurasa wa 5
Utekelezaji Endelezi wa Ajenda 'Nne Kuu' Kusaidia Kufufua Uchumi na Kuboresha Maisha ya Jamii

Ukurasa wa 8
Viwezeshaji vya Agenda 'Nne Kuu'

Ukurasa wa 14
Mpango wa Kuchochea Uchumi (Awamu ya Tatu)

Ukurasa wa 15
Matumizi ya Serikali

Ukurasa wa 16
Muhutasari wa Mapendekezo ya Ushuru

MADA YA BAJETI YA 2022/23 : "KUHARAKISHA KUFUFUA UCHUMI ILI KUBORESHA MAISHA YA WANANCHI"

Sheria ya 2012 inahitaji bajeti ya serikali kutangazwa kwa wananchi wote. Kwa sababu hiyo, lengo la Mwongozo huu wa Mwananchi ni kuwatangazia wananchi Bajeti ya Mwaka wa 2022/23.



Jumla ya Matumizi ya Serikali na Mikopo
Ksh. 3,342.8 bilioni

Matumizi ya Kawaida ya Wizara
Ksh. 1,387.9 bilioni
Matumizi ya Wizara kwa Maendeleo
Ksh. 711.5 bilioni
Malipo ya Faida na Pensheni
Ksh. 869.3 bilioni
Hazina ya Dharura
Ksh 4.0 bilioni
Mgao Haki kwa Kaunti
Ksh. 370.0 bilioni

BAADHI YA MATUMIZI MUHIMU:

Ajenda "Nne Kuu" na Nguzo zake

Ksh 10.1 bilioni
Kusaidia viwanda ili kutoa ajira.

Ksh 46.8 bilioni
Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe Bora kwa Wakenya wote.

Ksh 62.3 bilioni
Kuanzisha Bima ya Afya ili kuhakikisha huduma bora za matibabu kwa Wakenya wote na kwa bei nafuu.

Ksh 27.7 bilioni
Kutoa Nyumba Nzuri za Bei Nafuu kwa Wakenya wote.

Matumizi Mengine

Ksh 20.6 bilioni
Mpango wa Kuchochea Uchumi

Ksh 317.9 bilioni
Kuimarisha Usalama wa Kitaifa.

Ksh 368.5 bilioni
Kuendeleza Miundombinu ili kurahisisha shughuli za kiuchumi.

Ksh 513.8 bilioni
Kuzidisha juhudi za kutoa elimu bora kwa wengi.

Ksh 110.9 bilioni
Kulinda Mazingira, Maji na Mali Asili.

Ksh 69.0 billion
Usawa, Kupunguza Umaskini na Kuwezesha Wanawake na Vijana.

Ksh 15.6 billion
Kuimarisha Nyenzo za Habari,Mawasiliano na Tekinolojia.

Ksh 407.0 bilioni
Fedha kwa Serikali za Kaunti ambazo ni: Mgao Haki wa **Ksh 370.0** bilioni na Mgao wa Masharti wa **Ksh 37.0 bilioni**

Bajeti na Matumizi kwa Jumla

Jumla ya Mapato Ksh 2,447.0 bilioni

Ruzuku Ksh 33.3 bilioni

Upungufu (Ksh 862.5 bilioni)

Kufadhili Upungufu

Mkopo Kutoka Nje **Ksh 280.7 bilioni**
Mkopo Kutoka Nchini **Ksh 581.7 bilioni**

Kumbuka: Matumizi ya **Ksh 3,342.8 bilioni** ni kando na Fidia za **Ksh 702.5 bilioni.**

Sehemu za Mapato ya Jumla ya Ksh 2,447.0 bilioni pamoja na A.I.A



HALI YA **UCHUMI**

Uchumi uliimarika 2021 huku shughuli za kiuchumi zikiendelea kurejea hali ya kawaida kutokana na kulegezwa kwa masharti ya COVID – 19 na juhudi za Serikali zinazolenga kuchochea uchumi. Makadirio yanaonyesha kuwa uchumi utafufuka na kukua kwa asilimia 7.6 Mwaka wa 2021 baada ya kupugua kwa asilimia 0.3 mnamo 2020.

Katika Mwaka wa 2022, uchumi unakadiriwa kukua na kufikia kiwangp cha kadiri cha asilimia 6.0. Matokeo hayo yataimarishwa na utekelezaji wa miradi muhimu ya Serikali chini ya Ajenda "**Nne Kuu"** na juhudi zaidi chini ya Awamu ya Tatu ya Mpango wa Kuchochea Uchumi.

Uchumi unaendelea kuonyesha matokeo bora upande wa nyenzo kuu za kiuchumi. Mfumko wa bei umebakia katika kiwango kinachofaa huku viwango vya riba vya muda mfupi vikiwa chini na imara na mikopo kwa sekta ya kibinfasi ikiongezeka.

Mafanikio chini ya **Mpango wa Kuchochea Uchumi (ESP)**

Tangu kuingia nchini kwa ugonjwa wa COVID-19 mnamo 2020, Seikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Kuchochea Uchumi. Baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa chini ya mpango huu ni:

- **Maendeleo ya Miundombinu**; Ukarabati wa barabara na madaraja ya watu kupitia ili kuzidisha matumizi ya nyenzo za humu nchini na kutoa nafasi 200,000 za kazi kwa vijana chini ya Mpango wa "Kazi Mtaani".
- **Matokeo Bora ya Elimu**; Ujenzi wa madarasa zaidi katika shule za msingi na sekondari, kuajiriwa kwa walimu 1,000 wa kandarasi na wasomi 1,000 wa tekinolojia wanaojifunza ili kusaidia mafunzo ya kidijitali katika shule za serikali.
- **Uimarishaji wa Mapato ya Biashara**; Utoaji wa mtaji kupitia Mpango wa Kutoa Mikopo ili kuwezesha wenye biashara ndogo kupata mikopo. Hatua hiyo iliharakisha malipo ya kodi (VAT) na madeni mengine.
- **Matokeo Bora ya Afya**; Wafanyakazi 5,000 zaidi wa afya wa viwango vya diploma na cheti waliajiriwa.
- **Kilimo na Usalama wa Chakula**; Utoaji wa pembejeo za kilimo kwa bei nafuu kwa wakulima wadogo 200,000 na kuimarishwa kwa miradi ya kijamii ya unyunyizaji maji mashamba.
- **Utalii;** Ukarabati wa hoteli mbalimbali kwa mikopo yenye masharti nafuu iliyotolewa kupitia Shirika la Hazina ya Utalii na kuajiriwa kwa maskauti 5,500 wa Huduma za Wanyamapori Kenya.
- **Vifaa bora vya Usafi wa Mazingira na Maji**; Ukarabati wa visima vya maji, matangi ya maji chini ya ardhi, uvunaji zaidi wa maji ya mvua, na hatua za kukabiliana na kupunguza mafuriko.
- **Viwanda**; Ulivumisha sera ya "Nunua Kenya Ujenge Kenya", ukaendeleza shughuli za waundaji magari nchini na kutoa mikopo kwa Biashara Ndogo na za Kati katika sekta ya viwanda.
- **Ulinzi wa Jamii**; Utoaji wa fedha kwa walioathiriwa vibaya na makali ya janga la Corona mashambani na mijini.

Mafanikio ya Chanjo ya COVID-19

- Kufikia mwisho wa Machi, 2022, serikali ilikuwa imepokea chanjo milioni 27.1 na milioni 17.6 kati ya hizo zilikuwa zimetolewa.
- Kenya imepanga kutoa chanjo kwa raia watu wazima milioni 19 (ambao ni asilimia 70 ya idadi ya watu wazima) kufikia Juni 2022 ilhali waliobakia watakuwa wamepata chanjo hiyo kufikia mwisho wa mwaka.
- Sekta ya afya imetengewa **Ksh 7.0 bilioni** katika bajeti ya 2022/23, kugharamia utoaji chanjo asilimia 100 miongoni mwa miradi mingine katika sekta hiyo.
- Pesa zingine, **Ksh 100 milioni** zimetengewa Mpango wa Hatua za Dharura za COVID-19 Kenya na **Ksh 1.4 bilioni** za Mpango wa Utoaji Huduma na Uwekezaji Kenya (GESDeK) kuhusu COVID-19.

Mkenya akipokea chanjo ya COVID-19

UTEKELEZAJI UNAOENDELEA WA AJENDA “NNE KUU” KUSAIDIA KUFUFUA UCHUMI NA KUENDELEZA UKUAJI JUMUISHI

Mpango wa Ajenda “Nne Kuu” ulianzishwa na serikali miaka minne iliyopita kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kusaidia kutatua matatizo mbalimbali yanayokabili Wakenya.

Kutekelezwa kwa miradi iliyo chini ya Ajenda “Nne Kuu” ni hatua muhimu katika juhudi za kufufua uchumi, kutengeneza ajira, kusaidia shughuli za viwanda, kuimarisha huduma za afya, kuboresha usalama wa chakula na lishe bora na makao bora kupitia mpango wa serikali wa nyumba za bei nafuu.

Kwa sababu hiyo, **Ksh 146.8 bilioni** zimetengwa katika bajeti ya 2022/23 kutumika katika utekelezaji wa miradi muhimu chini ya Ajenda “Nne Kuu” kupitia Wizara, Idara na Mashirika mbalimbali:

1. Bima ya Afya Kwa Wote

Serikali imeweka mikakati ya uwekezeaji ambayo inapelekea nchi kufikia mpango wa Bima ya Afya Kwa Wote (UHC) na kuimarisha mfumo wa afya kukabiliana na milipuko ya magonjwa na changamoto nyingine za usalama wa kiafya ulimwenguni. Katika bajeti ya 2022/23 **Ksh 62.3 bilioni** zimetengewa Bima ya Afya Kwa Wote.

Baadhi ya pesa zilizotengewa sekta hiyo ni:

Ksh 5.2 bilioni	Huduma za Vifaa Vinavyosimamiwa
Ksh 4.1 bilioni	Huduma za Uzazi Bila Malipo
Ksh 1.9 bilioni	Bima ya Matibabu kwa wazee na walemavu sana katika jamii
Ksh 9.3 bilioni	Usambazaji wa Bima ya Afya Kwa Wote
Ksh 18.1 bilioni	Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta
Ksh 11.7 bilioni	Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi
Ksh 7.7 bilioni	Kituo cha Mafunzo ya Matibabu Kenya
Ksh 7.7 bilioni	Ushirikishi na Usimamizi wa Kitengo cha Bima ya Afya Kwa Wote
Ksh 5.2 bilioni	Chanjo
Ksh 1.2 bilioni	Ununuzi wa vifaa vya Upangaji Uzazi na Afya ya Uzazi
Ksh 900 milioni	Kubadilisha mifumo ya afya kulingana na Bima ya Afya Kwa Wote
Ksh 619.0 bilioni	Ununuzi wa vifaa katika Huduma za Kitaifa za Uongezaji Damu
Ksh 1.1 bilioni	Idara ya Hospitali ya Kitaifa ya Majeraha ya Moto na Magonjwa ya Watoto Kenya
Ksh 300 milioni	Ununuzi wa Vifaa vya Eksirei
Ksh 2.0 bilioni	Ujenzi na Uimarishaji wa Vituo vya Saratani
Ksh 16.2 bilioni	Hazina ya Kimataifa (Ukimwi, Malaria, Kifua Kikuu)

Kuandaa hospiatali kwa vifaa vya kisasa vya kimatibabu chini ya Mpango wa Huduma za Vifaa Vinavyosimamiwa (MES).

Rais Kenyatta akizindua Huduma za Afya Kwa Wote (UHC) katika Hospitali ya Port Reitz, Changamwe.

2. Kusaidia Viwanda Kuendelea Kutengeneza Ajira

Utekelezaji wa sera sahihi pamoja na uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda unaendelea kutoa matokeo mazuri na umesababisha mazingira yanayofaa ya kibiashara kwa ukuaji wa viwanda, utengenezaji ajira na maisha bora.

Katika bajeti ya 2022/23, **Ksh 10.1 bilioni** zimetengwa kusaidia viwanda vya humu nchini kupitia Wizara, Idara na Mashirika mbalimbali.

Kiwanda cha pamba kinatoa nafasi nyingi za kazi.

Kiwanda cha kisasa cha Rivatex East Africa Limited

Ksh 2.6 bilioni	Ujenzi wa Bandari Huru na Eneo la Viwanda Mombasa
Ksh 1.0 bilioni	Mpango wa Dhamana ya Mikopo
Ksh 3.0 bilioni	Kusaidia Ufikiaji wa Fedha na Ufufuaji wa Biashara.
Ksh 1.3 bilioni	Mradi wa Viwanda na Ujasiriamali Kenya
Ksh 626.0 milioni	Utoaji Fedha kwa Biashara Ndogo na za Kati katika sekta ya viwanda.
Ksh 200.0 milioni	Kituo cha Maendeleo ya Viwanda kwa Maeneobunge
Ksh 85.0 milioni	Ujenzi wa Eneo la Viwanda vya Nguo Naivasha
Ksh 142.8 milioni	Ustawishaji wa kiwanda cha pamba (RIVATEX) – msaada na upanuzi
Ksh 410.4 milioni	Kufanya kiwanda cha RIVATEX kuwa cha kisasa

3. Utoaji wa Nyumba Nzuri za Bei Nafuu kwa Wakenya wote

Serikali ilianzisha mpango wa kutoa nyumba nzuri na za bei nafuu kwa Wakenya. Kurahisisha mpango huo, serikali imeamua kuchukua mikopo kwa riba ya chini kutoka kwa sekta za umma na za kibinafsi ili kugharamia mradi mkubwa wa nyumba chini ya Mpango wa Nyumba za Bei Nafuu kupitia Hazina ya Kitaifa ya Ujenzi wa Nyumba na ushirika wa serikali na sekta ya kibinafsi.

Katika bajeti ya 2022/23, **Ksh 27.7 bilioni** zimetengewa Mpango wa Nyumba za

Bei Nafuu. Baadhi ya sehemu zilizotengewa fedha hizo ni:

Ksh 4.6 bilioni	Kuimarisha Kampuni ya Mikopo ya Rehani Kenya (KMRC);
Ksh 7.7 bilioni	Mradi wa Nyumba za Bei Nafuu (Kampuni ya Mikopo ya Rehani Kenya) ;
Ksh 1.0 bilioni	Ujenzi wa Nyumba za bei nafuu;
Ksh 5.9 bilioni	Mradi wa Kuboresha Mitaa Duni Kenya – Awamu ya II;
Ksh 1.05 bilioni	Nyumba za Polisi na Magereza Kenya;
Ksh 2.3 bilioni	Mpango wa Maendeleo Mijini Kenya (KenUP).
Ksh 1.2 bilioni	Ujenzi wa Makao ya Kijamii

4. Uimarishaji wa Usa… …akula na Lishe Bora kwa Wakenya wote

…nakula na lishe bora kwa Wakenya wote. Kupanuzi wa kilimo cha unyunyizaji maji …akula muhimu, upanuzi wa kilimo cha unyunyizaji maji …tekelezaji wa mipango ya kusaidia wakulima wadogo

…ewa mpango huu kama ifuatavyo:

Ksh 4.2 bilioni	Mradi wa Kitaifa wa Kilimo Vijijini
Ksh 1.5 bilioni	Mradi wa Kiwango Kidogo cha Unyunyizaji na Uongezaji Thamani
Ksh 1.7 bilioni	Mpango wa Kuimarisha Uzalishaji Nafaka Kenya
Ksh 1.9 bilioni	Hatua za Dharura za Kukabiliana na Nzige
Ksh 1.6 bilioni	Mradi wa Kitaifa wa Thamani ya Mazao;

Ksh 690 milioni	Mradi wa Usalama wa Chakula na Ukuzaji Mazao Mbalimbali
Ksh 7.0 bilioni	Mradi wa Kilimo Unaozingatia Hali ya Hewa
Ksh 1.1 bilioni	Awamu ya II ya Kufadhili Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
Ksh 2.6 bilioni	Mradi wa Maendeleo ya Biashara ya Ufugaji wa Samaki;
Ksh 2.8 bilioni	Mradi wa Uvuvi Baharini na Maendeleo ya Jamii Kiuchumi.
Ksh 1.3 bilioni	Utumiaji wa Rasilimali Hai Kwa Manufaa ya Kiuchumi.
Ksh 1.65 bilioni	Mpango wa Kuimarisha Biashara ya Mifugo Kenya.

Utekelezaji wa Mradi wa Kilimo Bunifu Kenya

Kuzidisha Mavuno kupitia Kilimo Bunifu

VIWEZESHAJI VYA AJENDA "NNE KUU"

A. Mazingira ya Kibiashara Yanayofaa kwa Uwekezaji

Uchumi Thabiti

Serikali inaendelea kudumisha uthabiti wa kiuchumi kupitia sera za kifedha zinazolenga kukuza uchumi, biashara, viwanda na utengenezaji ajira.

- Mfumko wa bei unaambatana na shabaha ya sera kwa kiwango cha asilimia 5±2.5 ilhali viwango vya riba viko chini na imara kuwezesha upatikanaji wa mikopo;
- Serikali pia imejitahidi kudumisha kiwango bora cha ubadilishaji fedha kuhakikisha kuna akiba ya kutosha ya kubadilishana fedha ili kujikinga dhidi ya mabadiliko ya ghafla katika masoko ya kimataifa;
- Akiba ya kubadilishana fedha katika Banki Kuu ya Kenya iko juu ya kiwango cha chini kinachotakiwa cha miezi 4.0 ya bima ya uagizaji ili kutoa kinga ya kutosha dhidi ya mabadiliko ya ghafla katika masoko ya kimataifa ya ubadilishanaji fedha.
- Kukamilisha sera yake ya kifedha, Serikali inaendeleza juhudi za kuimarisha hali yake ya kifedha kwa kuongezea mapato, kupunguza matumizi na kulipa madeni.

Uboreshaji wa Usalama wa Taifa

Usalama katika jamii ni muhimu katika kutimiza Ajenda "Nne Kuu" na miradi mingine ya kipaumbele. Kwa sababu hiyo, **Ksh 317.9 bilioni** zimetengewa mambo yafuatayo:

Ksh 10.7 bilioni	Ufadhili wa Kukodisha Magari ya Polisi;
Ksh 4.8 bilioni	Bima ya Matibabu kwa Maafisa wa Polisi na wa Magereza;
Ksh 2.3 bilioni	Bima ya Kibinafsi kwa Maafisa wa Polisi na wa Magereza;
Ksh 1.0 bilioni	Mfumo wa Kitaifa wa Mawasiliano na Upelelezi

Ksh 335.0 milioni	Ununuzi wa Vifaa vya Maabara ya Kitaifa ya Shughuli za Mahakama;
Ksh 1.0 bilioni	Huduma Namba.
Ksh 1.0 bilioni	Mpango wa Kuboresha Idara ya Polisi

Usajili wa maafisa zaidi wa polsi utaimarisha usalama

Kuboresha Mfumo wa Upelelezi wa Usalama Mijini

Matumizi ya Mfumo - Dijitali Kuchochea Uchumi

Serikali inaendelea kuwekeza katika miundombinu muhimu ya Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ili kuwezesha wananchi wengi kupokea habari kupitia kwa mtandao. Kutimiza lengo hilo, **Ksh 15.6 bilioni** zimetengwa katika bajeti ya 2022/23 kuboresha huduma za mtandao sehemu zote nchini.

Fedha hizo zimegawanywa kama ifuatavyo:

Ksh 5.2 bilioni	Ujenzi wa Miundombinu ya Mji wa Konza Awamu ya I;
Ksh 3.8 bilioni	Kituo cha Data cha Konza na Vifaa vya Mji huo;
Ksh 1.4 bilioni	Uwekaji wa Miundombinu ya Mtandao eneo la Eldoret-Nadapal
Ksh 70.0 milioni	Mradi wa Elimu Dijitali (Mpango wa Vipakatalishi Shuleni);
Ksh 620.0 milioni	Huduma za Pamoja za Serikali;
Ksh 2.7 bilioni	Utengenezaji na Ukarabati wa Miundombinu ya Mtandao katika Kaunti zote.
Ksh 682.0 milioni	Kuunganisha Mtandao katika mradi wa Ajenda “Nne Kuu”
Ksh 1.2 bilioni	Utengenezaji, Ukarabati na Upanuzi wa Mtandao Kaunti zote (NOFBI)

Kituo cha Kitaifa cha Data Konza

Serikali imeanza kuweka miundomsingi ya mtandao kuimarisha mawasiliano eneo la Kaskazini Magharibi

B. Ujenzi wa Miundombinu kwa Ukuaji Jumuishi

Ujenzi wa Barabara

Serikali inazingatia ujenzi na upanuzi wa barabara katika miji mikuu kote nchini ili kupunguza msongamano wa magari na kwa njia hiyo kupunguza gharama ya kufanya biashara.

Fedha zifuatazo zimetengwa katika bajeti ya 2022/23 kuboresha huduma za barabarani:

Ksh 103.7 bilioni	Ujenzi wa Barabara na Madaraja;
Ksh 42.1 bilioni	Ukarabati wa Barabara
Ksh 66.7 bilioni	Utengenezaji wa Barabara.

Ujenzi ukiendelea katika barabara ya Ruaraka - Outer Ring

Barabara Kuu ya Expressway, Nairobi, ambayo imekamilika

Ujenzi wa Reli na Bandari

Uchukuzi wa reli unazidi kuboresha usafiri na kupunguza msongamano katika barabara zetu. Kukamilishwa kwa Reli ya Kisasa ya SGR na kukarabatiwa kwa reli ya zamani kumeleta mfumo bora wa uchukuzi ambao ni salama, wa starehe na wa bei nafuu kwa abiria na mizigo.

Kutokana na juhudi za kuendelea kuboresha uchukuzi wa reli na ujenzi wa bandari, fedha zifuatazo zimependekezwa katika bajeti ya 2022/23 kugharamia kazi hiyo:

Bandari ya Mombasa inatoa ajira kwa wenyeji

- **Ksh 18.5 bilioni** za Reli ya SGR Nairobi – Naivasha awamu ya II
- **Ksh 9.1 bilioni** za Reli ya SGR Mombasa - Nairobi
- **Ksh 236 milioni** za mradi wa LAPSSET;
- **Ksh 2.6 bilioni** za Eneo Maalumu Kiuchmi la Dongo Kundu;
- **Ksh 1.0 bilioni** za Reli ya Riruta-Lenana-Ngong;
- **Ksh 450 milioni** za Reli ya Embakasi - Ruai;
- **Ksh 713 milioni** za ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini;

Kawi ya Kutegemwa

Kutimia kwa ajenda ya maendeleo ya nchi kutawezekana tu iwapo kutakuwa na huduma bora za kawi, za kutegemewa na za bei nafuu.

Kufikia lengo hilo, sekta hiyo imetengewa **Ksh 95.05 bilioni** katika bajeti ya 2022/23 kama ifutavyo;

Ksh 62.9 bilioni	Mfumo wa Kitaifa wa Umeme;
Ksh 18.5 bilioni	Uzalishaji wa Nguvu za Mvuke;
Ksh 9.3 bilioni	Usambazaji Umeme Vijijini;
Ksh 1.97 bilioni	Ustawishaji wa Nguvu za Kinuklia na Uchimbaji wa Makaa ya Mawe
Ksh 2.3 bilioni	Tekinolojia Badala za Kuzalisha Kawi

Kiwanda kipya cha kuzalisha kawi

Kiwanda cha Kawi ya Upepo katika Ziwa Turkana kinachotoa Megawati 300 za umeme

Usambazaji Bora wa Maji

Usambazaji wa maji safi na ya kutosha ni muhimu katika kutimiza mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Fedha za kutosha zimetengewa miundombinu ya maji na unyunyizaji, uondoaji majitaka na udhibiti wa mafuriko kwa usalama wa wananchi:

Ksh 45.9 bilioni	Ujenzi wa Miundombinu ya Maji na Uondoaji wa Majitaka;
Ksh 16.0 bilioni	Utunzaji wa Rasilimali za Maji;
Ksh 10.15 bilioni	Uhifadhi wa Misitu na Chemichemi za Maji;
Ksh 8.5 bilioni	Unyunyizaji na Ukombozi wa Ardhi;
Ksh 9.8 bilioni	Uhifadhi wa Maji na Udhibiti wa Chakula;
Ksh 6.05 bilioni	Kukabiliana na Hali ya Hewa
Ksh 7.0 bilioni	Uhifadhi na Utunzaji wa Wanyamapori;

Ujenzi wa Bwawa la Thiba

Ukarabati wa mtaro wa kusambaza maji

C. Kuendeleza Uwekezaji katika Huduma za Jamii kwa Ustawi wa Wakenya

Elimu Bora na Yenye Manufaa

Kwa lengo la kutoa elimu bora na yenye manufaa kwa Wakenya wote, serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha kwa sekta ya elimu ya msingi na sekondari.Fedha za seka hiyo katika bajeti ya 2022/23 ni kama ifuatavyo:

Ksh	**billion**
Ksh	**billion**
Ksh	**billion**
Ksh	**billion**
Ksh	**billion**
Ksh	**billion**



Serikali imetoa mafunzo kwa walimu zaidi ya 200,000 wa mfumo mpya wa elimu (CBC)

Usawa, Upunguzaji Umaskini na Msaada kwa Wanaoishi katika Mazingira Magumu

Serikali, chini ya Mpango wa Kitaifa wa Inua Jamii, inaendelea kusambaza manufaa ya uchumi bora kupitia msaada wa kifedha kwa wananchi wanaoishi katika mazingita magumu. Mgao katika bajeti ya 2022/23 ni kama ifuatavyo:

Ksh 17.5 billion	Fedha kwa Wazee;
Ksh 7.9 billion	Fedha kwa Mayatima na Watoto katika Mazingira Magumu;
Ksh 5.1 billion	Mpango wa Kukabiliana na Njaa
Ksh 1.2 billion	Fedha kwa Watu Walemavu Sana.
Ksh 500 million	Hazina ya Kitaifa ya Kukabiliana na Ukame
Ksh 2.6 billion	Mpango wa Kusaidia Waathiriwa wa Uhamisho Kenya.

Baadhi ya Walengwa wa Mpango wa Inua jamii

Fedha za kusaidia vijana na wanawake katika bajeti ya 2022/23

Ksh 2.2 billion	Mpango wa Kuwezesha Vijana kujiajiri;
Ksh 13.1 billion	Huduma ya Kitaifa ya Vijana (NYS);
Ksh 175 million	Hazina ya Kuimarisha Biashara za Vijana
Ksh 2.8 billion	Mradi Jumuishi wa Kijamii na Kiuchumi Kenya
Ksh 933.8 million	Shirika la Kutunza Watoto Kenya

Vijana wakifanya kazi katika eneo la Jua Kali chini ya Mpango wa Kuwezesha Vijana

Utekelezaji wa Mradi Jumuishi wa Kijamii na Kiuchumi Kenya (KSEIP); mipango ya Serikali ya kusaidia makundi mbalimbali (Hazina ya Kitaifa ya Serikali Kusaidia Wanaoishi Katika Mazingira Magumu (NGAAF), Hazina ya Wanawake ya Biashara (WEF) Hazina ya UWEZO, Michezo, Sanaa na Hazina ya Maendeleo ya Kijamii (SASDF) utasaidia kuleta usawa, kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya jamii hasa katika maeneo yaliyotengwa.

Bajeti ya 2022/23 imetenga fedha kwa miradi hiyo kama ifuatavyo:

Ksh 44.3 bilioni	Hazina ya Kitaifa ya Maeneobunge (NG-CDF);
Ksh 7.1 bilioni	Hazina ya Kukuza Usawa wa Kijamii;
Ksh 2.1 bilioni	Hazina ya Kitaifa ya Serikali Kusaidia Wanaoishi Katika Mazingira Magumu (NG-AAF).

Wanafunzi wakipokea msaada wa karo chini ya mpango NGAAF

Msaada kwa Wanawake katika sekta ya Jua Kali kupitia mpango wa WEF

D. Ufadhili kwa Kaunti Kuimarisha na Kuboresha Utoaji Huduma

Serikali ya Kitaifa imeendelea kufadhili Serikali za Kaunti kuhakikisha ugatuzi umefaulu.

Katika bajeti ya 2022/23, Serikali za Kaunti zimetengewa **Ksh 407.0** bilioni ambazo ni pamoja na:

- **Ksh 370.0 bilioni** Mgao Haki kutokana na Mapato ya Kitaifa;
- **Ksh 5.6 bilioni** Nyongeza yenye masharti kutoka kwa Serikali ya Kitaifa
- **Ksh 31.4 bilioni** mgao wenye masharti kutoka kwa Washirika wa Kimaendeleo.

Mgao Haki wa Ksh 370 bilioni kwa kila Serikali ya Kaunti

County	Equitable Share (Ksh billion)	County	Equitable Share (Ksh billion)	County	Equitable Share (Ksh billion)
Baringo	6.4	Kisumu	8.0	Narok	8.8
Bomet	6.7	Kitui	10.4	Nyamira	5.1
Bungoma	10.7	Kwale	8.3	Nyandarua	5.7
Busia	7.2	Laikipia	5.1	Nyeri	6.2
Elgeyo/Marakwet	4.6	Lamu	3.1	Samburu	5.4
Embu	5.1	Machakos	9.2	Siaya	7.0
Garisa	7.9	Makueni	8.1	Taita Taveta	4.8
Homa Bay	7.8	Mandera	11.2	Tana River	6.5
Isiolo	4.7	Marsabit	7.3	Tharaka Nithi	4.2
Kajiado	8.0	Meru	9.5	Trans Nzoia	7.2
Kakamega	12.4	Migori	8.0	Turkana	12.6
Kericho	6.4	Mombasa	7.6	Uasin Gishu	8.1
Kiambu	11.7	Muranga	7.2	Vihiga	5.1
Kilifi	11.6	Nairobi	19.2	Wajir	9.5
Kirinyaga	5.2	Nakuru	13.0	West Pokot	6.3
Kisii	8.9	Nandi	7.0		

MPANGO WA KUCHOCHEA UCHUMI (AWAMU YA TATU)

Kupitia mafanikio kutokana na awamu ya kwanza na ya pili ya Mpango wa Kuchochea Uchumi, serikali imeanzisha awamu ya tatu ya mpango huo inayolenga kuharakisha kukua kwa uchumi.

Katika awamu hii, Serikali itatenga fedha zaidi kutumiwa katika sekta **kumi na tatu** muhimu za uzalishaji na huduma ambazo ni: kilimo, afya, elimu, ukame, sera, miundombinu, ujumuishi kifedha, kawi na utunzaji mazingira.

Awamu hii imetengewa fedha zifuatazo katika bajeti ya 2022/23:

Ksh 2.1 bilioni	Mpango wa Kazi Mtaani
Ksh 4.0 bilioni	Ujenzi wa Madarasa ya CBC
Ksh 2.75 bilioni	Kuboresha Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari
Ksh 1.5 bilioni	Kuajiri walimu wa kandarasi na wasomi wa Tekinolojia wanaojifunza
Ksh 1.35 bilioni	Kuajiri wasomi zaidi wa afya wanaojifunza wa diploma na cheti
Ksh 5.8 bilioni	Kuboresha mazingira, maji na uondoaji majitaka
Ksh 1.5 bilioni	Ruzuku ya usambazaji wa pembejeo za kilimo
Ksh 1.0 bilioni	Mpango wa Dhamana na Mikopo
Ksh 604 milioni	Mikopo kwa Biashara Ndogo na za Kati (SMEs) katika sekta ya viwanda (KIE)

Mbolea ya bei nafuu kwa wakulima wadogo wa chai

Vijana wakifungua njia za majitaka mtaani Kibera chini ya Mpango wa Kazi Mtaani

MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI



MUHUTASARI WA MAPENDEKEZO YA KODI

Kodi ya Ongezeko la Thamani

- Magari yanayotengenezwa humu nchini yameondolewa kodi
- Pembejeo na malighafi za kutengeneza magari ya abiria zimeondolewa kodi
- Viwanda na mitambo ya kutengeneza dawa imeondolewa kodi
- Mafuta ya magari yameondolewa kodi
- Oksigeni ya matibabu, mifuko ya mkojo, nepi za watu wazima, matiti bandia, mifuko ya kolostomia na ileostomia imeondolewa kodi

Kodi ya Mapato

- Michango kwa mashirika yote ya ufadhili wa hisani haitatozwa kodi
- Huduma za Kidijitali zimeondolewa kodi cini ya vifungu 9(2) na 35 vya Sheria ya Mapato.
- Mashirika madogo ya kutoa mikopo yameondolewa kodi chini ya Sheria ya Mashirika Madogo ya Mikopo.
- Majengo yote ya kudumu Kenya yameondolewa kodi ya Huduma za Kidijitali.

Aina nyingine Kodi na Ada

- Kupunguzwa kwa ushuru wa uuzaji bidhaa nje kutoka 80% hadi 50%.
- Pembejeo na malighafi zinazoagizwa kutoka nje kutengenezea dawa zimeondolewa kodi.

Ushuru wa Bidhaa

- Mayai yayoagizwa kutoka nje ili kuanguliwa yameondolewa ushuru
- Spiriti ya kutengenezea dawa haitatozwa ushuru
- Magari yaliyotengenezwa humu nchini yameondolewa ushuru
- Viwango vya ushuru maalumu wa bidhaa vimeongezewa isipokuwa bidhaa za mafuta

Ukusanyaji Ushuru

- Jina la Mamlaka ya Ushuru Kenya limedabilishwa kuwa **Huduma za Ushuru Kenya**

MANENO YALIYOFUPISHWA

A.I.A	Hazina ya Kitaifa ya Msaada
CBC	Mtaala wa Elimu Unaozingatia Uwezo.
GJLO	Utawala, Haki, Sheria na Nidhamu
ICT	Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano
IDF	Ada ya Bidhaa Kutoka Nje
KMRC	Kampuni ya Dhamana ya Rehani Kenya
KNEC	Baraza la Kitaifa la Mitihani Kenya
LAPSSET	Bandari ya Uchukuzi Lamu Sudan Sudan Kusini na Ethiopia
MSME	Biashara Ndogo na za Kati
NG-CDF	Hazina ya Kitaifa ya Serikali ya Kustawisha Maeneobunge
NG-AAF	Hazina ya Kitaifa ya Serikali Kusaidia Makundi Yaliyotengwa
RDL	Ushuru wa Uchukuzi wa Reli
SEZ	Eneo Maalumu la Kiuchumi
SGR	Reli ya Standard Gauge
UHC	Huduma za Afya Kwa Wote
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani

TREASURY BUILDING, HARAMBEE AVENUE
P.O. BOX 30007 - 001000, Nairobi - Kenya Tel: +254 (0)20 2252299
Email: communications@treasury.go.ke Website: www.treasury.go.ke